**LEARNING BY EAR 2012**

# "Wasaliti walo karibu – Hadithi inayoangazia dhulma zinazoambatana na ngono"

**EPISODE 9: 'Bila sababu'**

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**
**EDITOR: Andrea Schmidt, Pendo Paul**
**PROOFREADER: Pendo Paul**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: SEREFA AND PATO AT HOME**

- **Pato (f, 16)**
- **Serefa (f, 40)**
- **Presenter (m, 25)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

**SCENE TWO: PATO AND SEREFA AT JUDY'S CENTRE**

- **Judy (f, 40)**
- **Serefa (f, 40)**
- **Narrator (m/f, around 30)**
- **2-3 women at the counselling center**

**SCENE THREE: PRECIOUS AND ALLAN AT HOME**

- **Precious (f, 30)**

- **Allan (m, 10)**
- **Presenter (m, 25)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

**<u>UTANGULIZI:</u>**

Nakusabahi na karibu katika kipindi cha **Noa bongo, Jenga maisha yako** ambacho mbali na kusikiliza pia unajifunza mambo kemkem. Hiki ni kipindi cha tisa katika hadithi inayoendelea ya, **'Wasaliti walo karibu',** tukiangazia maasi yanayoletwa na dhuluma za kingono. Kipindi kilichopita, mwanaharakati mkereketwa Judy alimuokoa Pato kutoka kwa mwalimu wake Bw. Maneno, aliyekuwa tayari kutaka kumdhulumu binti huyo kingono. Judy sasa ana azma ya kuipigia debe serikali iweke sheria kali dhidi ya dhulma za kingono. Sasa anawahamasisha waathiriwa katika kituo chake, wawe tayari kusema mikasa yao hadharani ili watu wajue ukweli wote. Nuru, hakutushangaza sisi tu bali hata nafsi yake, alipojitolea kuzungumzia mkasa wake hadharani. Lakini kwanza, yupo Uncle Joe aliyefungwa miaka mitano kwa kumlawiti Allan, kijana wa mpenzi wake Precious. Allan sasa anajitahidi kurudia maisha yake ya kawaida kwa usaidizi wa Bi. Rimba. Kipindi cha leo kinaitwa **'Sio sababu',** tunaanza alipo Pato na mamake Serefa nyumbani mwisho wa juma.

**<u>SCENE ONE: SEREFA AND PATO AT HOME</u>**

1. **SFX: KNOCK ON DOOR**

2. **PATO:** **(Pato enters, panting from jogging)** Habari, Mama!

3. **SEREFA:** Binti yangu, nafurahi maruhani yamekushuka sasa uko katika hali yako ya kawaida, Pato. Mazoezi

yalikuwaje?

4. **PATO:** Mazuri, natumai nitafikia matarajio yangu…

**SEREFA:** Pato, nimefurahi sana kwa kuweza kuzungumza kuhusu Bw. Maneno. Sikujua ni mtu muovu kiasi hicho! Dawa ya wanaume kama hao ni jela – au waondolewe uume wao kabisa!

5. **PATO:** **(shocked)** Mama!

6. **SEREFA:** Samahani, Pato – nina uchungu wa yale aliyokuwa akikufanyia – kwanini alikufanyia yote hayo. Nimekasirishwa sana, na nahisi vibaya kwamba sikuweza kugunduwa na kukusaidia mapema…

7. **PATO:** Tafadhali mama – yamekwisha hayo. Ninajaribu kuyasahau. Judy aliandikisha ripoti kwa askari polisi; wanaendelea na uchunguzi wao na mimi najaribu kujiondoa uoga nilionao. Ah – nimekumbuka. Nitahitaji kwenda kituoni kwake. Nilikwambia Judy anaandaa kongamano kubwa?

8. **SEREFA:** La? Kongamano la nini?

9. **PATO:** Judy anataka waathiriwa wa dhuluma za kingono waeleze visa vyao hadharani. Anafikiri hilo litaipa serikali changamoto ya kubuni sheria zinazoadhibu waasi wa dhuluma za kingono. Anataka sheria kali ndipo waasi wasithubutu kufanya tendo hilo.

**10. SEREFA:** Bila shaka hakukuomba ueleze watu kisa chako? Sidhani kama kuna haja ya kuwaeleza watu wengi kuhusu kisa chako.

**11. PATO:** La, mimi mwenyewe hakuniuliza. Lakini alitaka watu wajitolee. Nafikiri ni mwanamke mmoja aliyejitolea mpaka muda huu.

**12. SEREFA:** Pole, binti yangu, sikuwa nimeona ishara yeyote… labda kungelikuwa na mabadiliko... niambie, unahisi vipi sasa? Baada ya yote hayo kutokea? Unajimudu bado?

**13. PATO:** Sitaki kukumbuka, Mama. Naomba hilo tu. Nataka niendelee na maisha yangu, bila kukumbuka uahini huo.

**14. SEREFA:** Hmm… Naelewa. Pato, naahidi kukusaidia kwa lolote lile. Sasa nataka uende ukavuwe hizo nguo za majasho.

**15. PATO:** Yah, yah, najua… Mama, tafadhali kwanza washa redio? Tena tafuta stesheni yenye mziki mzuri… **(as she leaves)** Narudi sasa hivi.

**16. SFX: FOOTSTEPS LEAVE, RADIO TURNED ON**

**17. MTANGAZAJI:** … Na tangazo lilotufikia hapa kituoni ni hili: Shirika linalohamasisha watu kuhusu dhuluma za kingono limeandaa kongamano. Kongamano hili limeandaliwa wakati ambapo visa vya dhuluma hizi vimekithiri nchini. Waandalizi wametaka kuueleza umma athari ya visa hivi ambapo vimefikia asilimia 25 ya jumla ya idadi ya watu. Waathiriwa wanataka kuweka wazi na kuutaka umma uelewe, uwavumilie na uunge mkono vuguvugu hili. Shirika hili pia linataka kuishurutisha serikali ili kutunga sheria kali kwa waasi wa dhuluma za kingono na ubakaji. Baadhi ya wazungumzaji katika kongamano hilo ni…

**18. SFX: RADIO TURNED OFF**

**19. SEREFA:** **(disbelief)** Kwani nchi hii imeingia shetani gani?! Ni nani wakulaumiwa kuhusu haya? Kwani tulikosa nini kwa Mungu?

**20. PATO:** Nimerudi, Mama… Oh – kuna tangazo lolote zuri kwenye redio?

**21. SEREFA:** La… Sikiliza, unajua nini? Ni muhimu kwenda kukutana na Judy. Mimi binafsi nitakupeleka.

**22. PATO:** Mama, uko sawa? Unaonekana kama umeshtuka!

**23. SEREFA:** Bila shaka... siamini ninayosikia… harakisha, Pato. Hebu twende.

24. **MSIMULIZI:** Serefa siye pekee anayejiuliza haya maswali. Wengi hawaelewi ni kwa nini dhulma za kingono zimekithiri nchi nyingi barani Afrika. Imekuwa ni mila? Je ni kwa sababu jamii za Kiafrika zimewapa wanaume mamlaka na nguvu nyingi kuliko wanawake? Serefa hajaamini kuwa binti yake amewahi kudhulumiwa kingono na mwalimu wake, Bw. Maneno. Lakini baada ya kusikia hayo matangazo redioni aliamua kumsindikiza binti yake Pato, katika shirika analofanya kazi Judy.

**SCENE TWO: PATO NA SEREFA KITUONI**

25. **SFX: FEMALE VOICES COMPLAINING AND MURMURING**

26. **JUDY:** Vyema… Sote tuko tayari kwa mkutano? Vizuri. Nyote mnakaribishwa. Labda mmoja wenu atueleze unatakiwa kufanya nini unapojikuta mahali ambapo una hofu?

27. **SEREFA:** **(clears throat)** Em - Samahani… jina langu ni Serefa - mamake Pato. Siko hapa kwa sababu kama mlizo nazo nyinyi – nimemleta binti yangu – lakini nilitaka kusema kuwa sikuwahi kujua kuwa maasi haya ni mengi sana nchini.

28. **JUDY:** Kwa kweli, yako mengi maasi kuliko tunavyojua. Waathiriwa wengi wanajificha. Unajua kuwa, kwa mfano, Afrika kusini, takriban wanawake 150 hamsini wanabakwa kila siku?

**29. SEREFA:** **(shocked)** Ati nini? Haiwezekani!… Wanawake wanaishi vipi huko?

**30. JUDY:** Swali zuri. Lakini sio huko tu kwenye hofu barani Afrika. Sehemu moja ya Kongo ndiyo yenye matukio ya kinyama zaidi ya dhuluma za kingono. Kuna takriban watu laki mbili ambao ni waathiriwa wa dhuluma za kingono nchini Demokrasia ya Kongo. Wote hao ni manusura wa ubakaji.

**31. SEREFA:** **(shocked)** Hapana! Watu 2000 manusura wa ubakaji? Na nilifikiria Pato yuko peke yake… poleni ,sikutaka kuchukua muda wenu mwingi – nilikuwa nimemleta Pato kwa sababu…

**32. JUDY:** Ulihofu chochote kingine kinaweza kutokea? Au hata kukutokea wewe? Nafahamu. Sote twahofia. Swali ni, tutajikinga vipi?

**33. SEREFA:** Sijui… nili…ninataka mwanangu akue katika mazingira salama na yanayochungwa. Hayo tu ndiyo naweza kusema kwa sasa.

**34. JUDY:** Basi njoo ujiunge nasi katika kongamano! Twahitaji kila mtu. Vita hivi ni vyetu sote. Ni vita vyakuboresha jamii- kila mtu sharti apigane.

**35. MSIMULIZI:** Judy hakuchoka kueleza umuhimu wa kujisimamia. Alieleza maafa yatakayodumu licha ya kuwa tendo hilo limetokea mara moja maishani mwa mtu. Serefa alipewa nasaha ya kutokuwa kando na binti yake wakati kama huu. Waathiriwa ili kujenga tena uaminifu wanahitaji watu wao wa karibu kuwa nao bega kwa bega. Kwa sasa, Precious yuko nyumbani anamuandalia chakula Allan. Allan pia, ameanza kumtembelea Judy kwa ushauri. Amemaliza kumuandikia kazi aliyokuwa amemuahidi kumsaidia, na sasa ameketi anasikiliza redio.

**<u>SCENE THREE: PRECIOUS AND ALLAN AT HOME</u>**

**36. SFX: MUSIC INTERLUDE.....INTERRUPTED**

**37. MTANGAZAJI:** Habari tena – tunakatiza muziki ili kukupa taswira ya wingu la uasi la dhuluma za kingono lililoenea nchini. Kulingana na habari zilizotufikia hivi punde, Shoka, mkuu wa waasi anayejulikana kwa kupanga ubakaji wa makundi, mateso na dhuluma nyengine, ametiwa mbaroni hii leo. Shoka pia, anatakiwa na Mahakama ya Kimataifa yaani International Criminal Court (ICC) kwa makosa ya jinai, na atafikishwa mahakamani juma lijalo. Tutazidi kukuletea habari kwa umakini mkubwa, kwa sasa: pata kibao hicho.

**38. SFX: MUSIC INTERLUDE**

**39. ALLAN:** **(shouts)** Mama! Mamaaa! Wamewatia mbaroni waasi. Wamesema sasa hivi redioni.…

**40. PRECIOUS:** Oh, habari njema, mwanangu! Watu wote wale wanaoishi mipakani haswa wanawake… sasa hawatakuwa tena na haja na kuhofia. Njoo mezani, nishaandaa chakula. Na uwe tayari kwenda kumuona Judy. Umemaliza kumuandikia kazi yake?

**41. ALLAN:** Ndiyo.

**42. PRECIOUS:** **(fondly)** Nakupenda sana, Allan.

**43. ALLAN:** Mama… bado naumwa na tumbo…

**44. PRECIOUS:** Najua mwanangu… daktari alisema maumivu yatachukua muda kumalizika. Lakini karibuni yataisha, nakuahidi utapona. Njoo – njoo tule. Nimekupikia chakula ukipendacho! Na ukimaliza tu tutakwenda kituoni kwa Judy, La sivyo tutachelewa.

**45. ALLAN:** **(starting to eat)**

**<u>HITIMISHO:</u>**

Allan anapojibugia chakula hicho ndipo tunapohitimisha kipindi chetu cha tisa cha masuala ya dhuluma za kingono barani Afrika. Kweli Judy atafaulu kuipa serikali msukumo kuhusu sheria hizo mpya za dhuluma za kingono? Na Nuru ataweza kuyazungumzia maasi aliyofanyiwa wakati wa ubakaji wake? Na je, Pato atakuwa salama shuleni mwake, hivi ambapo Bw. Maneno amejiuzulu? Pata haya katika kipindi chetu cha mwisho.

Kumbuka kutazama au kutuma maoni katika wavuti wetu: dw.de/lbe. Au mtandao wetu wa Facebook. Tukutane tena, kwaheri.